*Bismillahir Rahmanir Rahim*

# VUCHAMA UGWENO ISLAMIC SECONDARY SCHOOL

**P.O. BOX 10 VUCHAMA -MWANGA-KILIMANJARO MOB: 0713-444438**
www.vuchamaislamic.ac.tz email:vuchamaugwenoislamic26@gmail.com.

PASSPORT SIZE OF STUDENT/

PICHA YA MWANAFUNZI

## APPLICATION FORM FOR ACADEMIC YEAR 2024

**A. STUDENT'S GENERAL INFORMATION:**

**FULL NAME:** ____________ ____________ ____________

JINA KAMILI (FIRST NAME/JINA LA KWANZA) (MIDDLE NAME/JINA LAKATI (SUR NAME/JINA LA UKOO)

**DATE OF BIRTH:** ____________
TAREHE YA KUZALIWA DATE/MONTH/YEAR

**GENDER** JINSIA **MALE** MVULANA ☐ **FEMALE** MSICHANA ☐

**NATIONALITY**/UTAIFA: ____________________________________________

**HOME ADDRESS**/MAKAZI: ____________________________________________

**PREVIOUS SCHOOL**/SHULE ULIYOTOKA: ____________________________________________

**CLASS REQUESTED:** ____________________
DARASA UNALOINGIA:

**DAY** KUTWA ☐ **BOARDING** BWENI ☐

**B. PARENT'S INFORMATION:**
**TAARIFA YA MZAZI**

**FATHER** / BABA
**FULL NAME:** ____________ ____________ ____________
JINA KAMILI (FIRST NAME / JINA LA KWANZA) (MIDDLE NAME / JINA LA KATI) (SURNAME / JINA LA UKOO)

PASSPORT SIZE OF FATHER

PICHA YA BABA

**NATIONALITY**/UTAIFA: ____________________________________

**HOME ADDRESS**/MAKAZI: ____________________________________

**PHONE NUMBER** / NAMBA YA SIMU: ____________________________

**WORK** / KAZI: ____________________________________________

## C. PARENT'S INFORMATION:
TAARIFA YA MZAZI:

**MOTHER** / MAMA
**FULL NAME:**
JINA KAMILI

| | | |
|---|---|---|
| | | |
| (FIRST NAME / JINA LA KWANZA) | (MIDDLE NAME / JINA LA KATI) | (SURNAME / JINA LA UKOO |

**NATIONALITY**/UTAIFA: ______________________________________________

**HOME ADDRESS**/MAKAZI: ___________________________________________

**PHONE NUMBER** / NAMBA YA SIMU: ________________________________

**WORK** / KAZI: ____________________________________________________

PASSPORT SIZE OF MOTHER/

PICHA YA MAMA

**DECLARATION:**

I declare that to the best of my knowledge the above particulars are correct and complete, I am aware that any false statement(s) will lead to this registration being rejected or to the annulment of admission already granted and may also render me liable to prosecution under the laws of the Government of United Republic Of Tanzania.

***Parent / Sponsor / Guardian Name:*** ______________________________________________

***Date:*** _________________________________ ***Signature:*** ______________________________

**TAMKO:**

Nakiri kuwa kwa uelewa wangu wa hali ya juu nimesoma maelezo yote na kuyaelewa vizuri na taarifa nilizozitoa ni za kweli kabisa na kama ikithibitika si za kweli nichukuliwe hatua za kisheria kutokana na Sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

***Jina la Mzazi / Mdhamini / Ndugu:*** _______________________________________________

***Tarehe:*** ________________________________ ***Sahihi:*** _______________________________

# MEDICAL EXAMINATION FORM

**This Form should be completed by a Registered Medical Officer or Doctor**

Full name of student ……………………………………………………………Age…………………….

Health history……………………………………………………………………………………………..

Audiometric (hearing) screening………………………………………………………………………

Nutritional Assessment…………………………………………………………………………………

TB Risk Assessment and Test…………………………………………………………………………

Blood Test (for anemia)…………………………………………………………………………………

Blood group …………………………… BP …………………………………………………………….

Urine test……………………………………………………………………………………………………

Stool Examination…………………………………………………………………………………………

Breathing System ………………………………………………………………………………………

Skin ………………………………………………………………………………………………………….

Visual Test…………………………………………………………………………………………………

Asthma ……………………………………………………………………………………………………….

**Additional Information:-**
Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases if any…………………

……………………………………………………………………………….

I declare that all the information provided herein is true to the best of my knowledge

Name……………………………………………………………………………………………………

Signature…………………………..

Designation………………………..

Date………………………………………………….. Official stamp…………………………………………..

**Note:**

*Student should bring the Completed form to school/ Mwanafunzi ailete fomu hii shuleni ikiwa imejazwa.*

***This Form Costs TShs. 10,000/= (Non – Refundable)***

***Kwa Mawasiliano Zaidi: Manager wa Shule Simu: 0713 136842 / Mkuu wa Shule Simu: 0713 444438***

***Bismillahir Rahmanir Rahim***

# VUCHAMA UGWENO ISLAMIC SECONDARY SCHOOL

**P.O. BOX 10 VUCHAMA -MWANGA-KILIMANJARO Mob: 0713 136842 Mob: 0713444438 / 0673 444439**

**www.vuchamaislamic.ac.tz Email:Vuchamaugwenoislamic26@gmail.com.**

## JOINING INSTRUCTION

KUMB.NA.VUISS/VOL.24………. DATE: ……………………..

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI: ………………………………………………………….

S.L.P ……………………………………………………………………………………………

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI YA KIISLAMU VUCHAMA UGWENO, ILIYOPO WILAYA YA MWANGA, MKOA WA KILIMANJARO MWAKA 2024**

### 1.0. PONGEZI

Nafurahi kukutaarifu kuwa Mwanao amechaguliwa Kujiunga na Kidato cha …….. katika Shule ya Sekondari ya Kiislamu Vuchama Ugweno Mwaka 2024. Shule ipo umbali wa Kilometa **29 kutoka Mji wa Mwanga.** Shule ipo Wilaya ya Mwanga, Mkoa wa Kilimanjaro.

Ukiwa Mwanga/ Arusha/ Moshi panda Magari ya Ugweno Vuchama Ngofi. Gari litakufikisha moja kwa moja Shuleni na ukiwa Dar es Salam/ Pwani panda basi la **Mvungi Safari** litakufikisha moja kwa moja Shuleni na zaidi ya hapo wasiliana na Uongozi wa Shule kwa Namba za Simu zilizotajwa hapo juu. Muhula wa Masomo utaanza tarehe. **08-01-2024** Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti Shuleni tarehe.**07-01-2024** Mwisho wa kuripoti ni tarehe **31/01/2024.**

Endapo Mwanafunzi hatoripoti hadi tarehe hiyo ya mwisho itahesabika kuwa amepoteza nafasi hiyo na itajazwa kwa kufuata taratibu za uchaguzi wa wanafunzi wanaochaguliwa kujiunga na Shule ya Vuchama Ugweno. Jitahidi kuripoti saa **1:30 asubuhi** hadi saa **12:00 jioni** ili kuondoa usumbufu unaoweza kujitokeza.

**2.2: ADA NA MICHANGO YA SHULE:**

a) Ada ya Shule kwa Mwaka ni **Shilingi 2,000,000/= (Bweni)** na **Kutwa Shs**. **1,000,000/=** Ada inalipwa kwa **Awamu Nne (4)** tu.

Fedha hizo zinalipwa kwenye Akaunti ya Shule, Na. **40210004844** tawi lolote la **NMB Shs. 1,720,000/= ada kwa mwaka** na akaunti ya hostel **Na. 21210049548** tawi lolote la **NMB shs. 280,000 hostel kwa mwaka** kwa jina la vuchama ugweno Islamic secondary school.

b) Malipo yalipwe benki, halafu nakala ya Malipo **(pay in slip**) iwasilishwe shuleni ofisini kwa mhasibu.

**NB:** Hakikisha unaandika jina la Mwanafunzi kwenye banki **Pay-in-Slip** ya malipo ya ada au michango ya mwanafunzi husika.

c) Malipo yanayotakiwa kulipwa na kila Mzazi/Mlezi ni kama inavyoelekezwa kwenye majedwali yaliyo ambatanishwa mwishoni mwa form hii;

# KIAMBATANISHO CHA MALIPO

**MALIPO YA ADA NA MICHANGO YAKE KWA MWANAFUNZI WA BWENI KWA MWAKA**

| | MICHANGO | WAVULANA | WASICHANA | MAELEZO | A/C NO |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ADA | **1,720,000** | **1,720,000** | Lipia Benki | **40210004844** |
| 2 | BWENI | **280,000** | **280,000** | Lipia benki | **21210049548** |
| 3. | VITABU | **120,000** | **120,000** | Lipia Benki | **40210004844** NMB JINA: VUCHAMA UGWENO ISLAMIC SEC |
| 4. | UCHAKAVU | **100,000** | **100,000** | Lipia Benki | |
| 5. | SARE ZA SHULE | **135,000** | **175,000** | Lipia Benki | |
| 6. | KITAMBULISHO | **5,000** | **5,000** | Lipa Benki | |
| | **JUMLA YA MALIPO** | **2,360,000** | **2,400,000** | Lipia Benki | |

**MALIPO YA ADA NA MICHANGO YAKE KWA MWANAFUNZI WA KUTWA KWA MWAKA**

| | MICHANGO | WAVULANA | WASICHANA | MAELEZO | A/C N0 |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | ADA | **1,000,000** | **1,000,000** | Lipia Benki | **40210004844** NMB JINA: VUCHAMA UGWENO ISLAMIC SEC |
| 2. | VITABU | **120,000** | **120,000** | Lipia Benki | |
| 3. | UCHAKAVU | **100,000** | **100,000** | Lipia Benki | |
| 4. | SARE ZA SHULE | **135,000** | **175,000** | Lipia Benki | |
| 5. | KITAMBULISHO | **5,000** | **5,000** | Lipa Benki | |
| | **JUMLA YA MALIPO** | **1,360,000** | **1,400,000** | Lipia Benki | |

**MICHANGO MINGINE MUHIMU YA SHULE 2024**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | MITIHANI **(kidato cha nne)** | **150,000** | Lipia Benki | **40210004844** NMB JINA: VUCHAMA UGWENO ISLAMIC SEC |
| 8. | MITIHANI (**kidato cha pili** ) | **90,000** | Lipia Benki | |

**NB**:

a) *Fedha ikishalipwa haitarejeshwa.*
b) *Shule itatoa Huduma ya Kwanza ya matibabu (**First Aid**) na baada ya hapo Mzazi / Mlezi atawajibika pale inapohitajika huduma zaidi ya kimatibabu*
c) *Ukileta watoto wako wawili wa familia moja unapata punguzo la **10%** ya ada kwa mtoto mmoja wakiwa wote shuleni.*
d) *Safari za masomo (**study tour**) zitatangazwa gharama zake pindi zitakapo fanyika.*

| MCHANGANUO WA MALIPO YA ADA KWA AWAMU NNE KWA MWAKA 2024 | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **AWAMU YA KWANZA** | **BWENI WAVULANA** | | **BWENI WASICHANA** | | **AKAUNTI YA KULIPIA- NMB** |
| **JANUARY** | ADA | **430,000** | ADA | **430,000** | 40210004844 |
| | HOSTEL | **70,000** | HOSTEL | **70,000** | 21210049548 |
| | VITABU | **120,000** | VITABU | **120,000** | **40210004844** NMB AKAUNTI ZOTE JINA: VUCHAMA UGWEN0 ISLAMIC SECONDARY |
| | UCHAKAVU | **100,000** | UCHAKAVU | **100,000** | |
| | SARE | **135,000** | SARE | **175,000** | |
| | KITAMBULISHO | **5,000** | KITAMBULISHO | **5,000** | |
| **JUMLA** | | **860,000** | | **900,000** | |

| **AWAMU YA KWANZA** | **KUTWA WAVULANA** | | **KUTWA WASICHANA** | | **AKAUNTI YA KULIPIA- NMB** |
|---|---|---|---|---|---|
| **JANUARY** | ADA | **250,000** | ADA | **250,000** | **40210004844** NMB AKAUNTI ZOTE JINA: VUCHAMA UGWEN0 ISLAMIC SECONDARY |
| | VITABU | **120,000** | VITABU | **120,000** | |
| | UCHAKAVU | **100,000** | UCHAKAVU | **100,000** | |
| | SARE | **135,000** | SARE | **175,000** | |
| | KITAMBULISHO | **5,000** | KITAMBULISHO | **5,000** | |
| **JUMLA** | | **610,000** | | **650,000** | |

| AWAMU YA PILI | BWENI WAVULANA | BWENI WASICHANA | AKAUNTI YA KULIPIA- NMB |
|---|---|---|---|
| **APRIL** | ADA 430,000 | ADA 430,000 | **40210004844** |
| | HOSTEL 70,000 | HOSTEL 70,000 | 21210049548 |
| | **JUMLA 500,000** | **JUMLA 500,000** | |
| | **KUTWA WAVULANA** | **KUTWA WASICHANA** | |
| | ADA 250,000 | ADA 250,000 | **40210004844** |
| **AWAMU YA TATU** | **BWENI WAVULANA** | **BWENI WASICHANA** | **AKAUNTI YA KULIPIA- NMB** |
| **JULY** | ADA 430,000 | ADA 430,000 | **40210004844** |
| | HOSTEL 70,000 | HOSTEL 70,000 | 21210049548 |
| | **JUMLA 500,000** | **JUMLA 500,000** | |
| | **KUTWA WAVULANA** | **KUTWA WASICHANA** | |
| | ADA 250,000 | ADA 250,000 | **40210004844** |
| **AWAMU YA NNE** | **BWENI WAVULANA** | **BWENI WASICHANA** | **AKAUNTI YA KULIPIA- NMB** |
| **SEPTERMBER** | ADA 430,000 | ADA 430,000 | **40210004844** |
| | HOSTEL 70,000 | HOSTEL 70,000 | 21210049548 |
| | **JUMLA 500,000** | **JUMLA 500,000** | |
| | **KUTWA WAVULANA** | **KUTWA WASICHANA** | |
| | ADA 250,000 | ADA 250,000 | **40210004844** |

**NB:**
***Nakala hii ya mejedwali ya malipo ni mali ya mzazi/mlezi, tafadhali baki nayo***

**UTARATIBU WA KULIPA FEDHA NA MAHITAJI YA SHULE (ADA NA MAHITAJI MENGINE):-**

Tafadhali Lipa fedha na Mahitaji ya Shule wiki moja kabla ya Shule kufunguliwa, usitume fedha kwa njia ya Simu au kulipa Cash shuleni **(kufanya hivyo hairuhusiwi, na upotevu wowote wa fedha kwa njia hizo shule haitahusika) ufafanuzi zaidi piga simu 0673 444439**

**AGIZO:**

i) Siku ya kuripoti hakikisha unaleta nakala ya malipo (**Bank Pay-in-Slip)** na kuikabidhi kwa Mhasibu ili akupatie risiti ya shule ndipo mwanafunzi apokelewe. Tayari kuelekea kwa Patron au Matron kwa ukaguzi mwingine.

ii) Fika shuleni ukiwa na nakala (copy ya cheti cha kuzaliwa).

iii) Fika na uhamisho kama unahamia.

## 2.0: SARE ZA SHULE:-

### 2.1: Sare za Shule Zinazopatikana Shuleni:

a) **Kwa Wasichana:** Ni gauni mbili (2), suruali mbili (2), juba nyeupe mbili (2), sweta la shule moja.

b) **Kwa Wavulana:** Suruali mbili (2), nusu kanzu nyeupe mbili(2), sweta moja, na T-shirt za shule mbili (2).

### 2.2: Sare Anazotakiwa Kuja Nazo Kutoka Nyumbani:

**a) Kwa Wasichana**:

**i) Sare za michezo**: *Track suiti moja ya bluu bahari (**light blue**) soksi jozi nne nyeusi na viatu (raba nyeupe) vya michezo*

**ii) Sare za kushindia**: Juba jeusi, baibui jeusi na suruali yake(1), Juba,baibui na suruali yake rangi ya **karoti** kitambaa cha Suti (***ISTEM***) na kisiwe cha mpira, Nguo za ndani za kutosha na jozi ya kitenge kwa wasichana, Viatu vya shule ni vya ngozi vyeusi vya kufunga kwa kamba vyenye kisigino kifupi, Soksi jozi mbili nyeupe ndefu na mbili nyeusi, Dera moja,sweta la kijivu shingo ya **V** mikono mirefu na sandles au yeboyebo rangi nyeupe.

**NB*:*** *Skintight ndefu haziruhusiwi kwa wasichana, Aje na nguo za ndani za kutosha ili kuruhusu ukaukaji wa nguo nyingine.*

- *Kitambaa cha karoti kimeambataniswa na form hii.*

b) **Kwa Wavulana**:

i) **Sare za michezo**: *Track suit nyeusi (black) soksi jozi mbili nyeusi na viatu (raba nyeupe) vya michezo.*

ii) **Sare za kushindia**: Suruali nyeusi 2 za kitambaa chini ziwe (*upana inch 15*),na sweta 1 la kijivu shingo ya **V**-mikono mirefu, ***Kanzu nyeupe na Kofia nyeupe*** (kuvaa siku ya Ijumaa) soksi nyeupe jozi 2 na viatu vya shule vyeusi vya kamba.sandles au yeboyebo rangi nyeusi.

c) **Mahitaji Muhimu Ambayo Mwanafunzi Anapaswa Kuleta Shuleni ni:**

1. Ream ya Karatasi **A4** (1) kwa Term,kwa mwaka Ream **2**,aina ya **aØne** au **Double A**
2. Madaftari makubwa (Counter Books-Quire 3) kumi na tatu (**15**).
3. Flat spring File za Plastic 2.
4. Rulled Paper bando 1. (kwa term) mbili kwa mwaka.
5. Graph Pad 1.
6. Mas-haf (1) chapa ya saudia.
7. Kopo la Vifaa vya Hisabati (Mathematical Set Instruments).
8. Kalamu za Wino 4,pencils 4 , Rula 1na Kifutio 2.
9. Ndoo mbili (2) zenye mifuniko (kubwa 1 ndogo 1).
10. Shuka mbili (2) rangi ya **Blue bahari,** Blanketi(1) rangi ya **kijivu** moja (1), Chandarua pembe nne ya futi (4x6) rangi **nyeupe** moja(1).
11. Mwanafunzi aje na Sanduku la bati (trunker) lenye kufuli kwa ajili ya kuhifadhia vitu vyake.
12. Shule haina Chakula maalumu ***(special diet)*** Mzazi / Mlezi anajukumu la kuona ni jinsi gani mtoto / watoto wao wenye mahitaji maalumu ya chakula watakavyohudumiwa.
13. Mafuta ya kujipaka ya mgando, Dawa ya Meno, Mswaki, Ndala, Taulo, na Dawa ya Viatu (Kiwi nyeusi).

**NB:** ***Baaadhi ya vitu vilivyoorodheshwa hapo juu unaweza kuja kuvinunua katika Duka la Shule isipokuwa Sanduku la bati (Trunker) na viatu.***

**ZINGATIO:**

a) Ni marufuku Mwanafunzi kuja na Simu ya Mkononi, Pasi ya Umeme, au Heater na manukato ya aina yoyote hapa Shuleni.

b) Aje akiwa amevaa sare za shule ama sare za kushindia kama zilivyotajwa hapo juu.

c) **Muda:**

- Muda wa kuripoti ni Kuanzia saa **1:30 asubuhi.**
- Mwisho wa kuripoti ni saa **12:00 jioni**.

## SHERIA, KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE:-

Shule inaendeshwa kwa Mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya Mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya Mwaka 1995. Aidha, inazingatia Miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi yenye Dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais TAMISEMI yenye Jukumu la Usimamizi na Uendeshaji Elimu (Sheria hizi zipo kwenye Kiambatanisho )

**MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria Masomo kwa siku **90** (Tisini) bila taarifa yoyote shule/ utoro;
iii. Kugoma au kuhamasisha mgomo shuleni au nje ya shule;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, Walimu / Walezi na Jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga Mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalika na uongozi wa shule (ambao ni nywele tano);
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa Pombe na matumizi ya Madawa ya kulevya;
ix. Uvutaji wa Sigara / Bangi na vinginevyo;
x. Uasherati, Uhusiano wa Jinsia moja, Kuoa au Kuolewa;
xi. Kupata Ujauzito au kutoa Mimba;
xii. Kushiriki matendo ya Uhalifu, Siasa na Matendo yoyote yale yanayovunja Sheria;
xiii. Kusababisha Mimba au kumpa mtu Mimba;
xiv. Kutembelea Majumba ya Starehe na Nyumba za Kulala Wageni;
xv. Kumiliki au kukutwa na Simu ya Mkononi katika Mazingira ya Shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la Kujiua, au Kutishia kujiua kama kunywa Sumu n.k
xviii. Uharibifu wa Mali za Shule au za Umma kwa makusudi.

***KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI YA KIISLAMU VUCHAMA UGWENO***

## SHERIA ZA SHULE:-

1. Mwanafunzi anapaswa kutekeleza Ibada / Swala zote kulingana na Ratiba ya Shule ilivyopangwa.
2. Mwanafunzi anapaswa kuwepo eneo la shule wakati wote isipokuwa anapopata ruhusa maalum kutoka kwa mwalimu wa zamu,Makamu Mkuu wa shule au Mkuu wa shule.
3. Mwanafunzi anapaswa kuvaa Sare ya Shule muda wote wa Shule (darasani), wakati wa kutoka nje ya shule, wakati wa kwenda likizo na kurudi. Muda wa kazi za mikono na michezo mwanafunzi atavaa nguo rasmi za kazi / michezo.
4. Kuchelewa kurudi shuleni wakati wa kutoka likizo hata kwa siku moja (1) ni kosa kubwa. Ikitokea Mwanafunzi akachelewa aje ameambatana na Mzazi / Mlezi.
5. Mwanafunzi anapaswa kutii,kuheshimu na kuthamini kazi za darasani na nje ya darasa muda wote. Kazi za darasani ni pamoja na kufanya Mazoezi, Majaribio ya wiki na/mwezi, Mitihani Robo Muhula, Nusu Muhula na Mitihani ya Muhula.
6. Mwanafunzi atakaye bainika kufanya udanganyifu katika mitihani ya ndani na nje ya shule, atafutiwa matokeo na mzazi atagharamia maandalizi ya mtihani mwingine.
7. Mgeni anayemtembelea mwanafunzi kamwe haruhusiwi kuleta chakula Kilichopikwa (Mfano: Pilau, Wali, Nyama, Chapati n.k) .Hii itazuia uwezekano wa kusababisha magonjwa ya tumbo, kuhara, kipindupindu n.k). Ukija nacho utarudishwa nacho.
8. Kutii Uongozi na Viongozi ni Wajibu wa kila Mwanafunzi. Mwanafunzi anapaswa Kuheshimu Uongozi na Utawala wa Shule, Walimu na Wafanyakazi wasio-Walimu, Uongozi wa Serikali ya Wanafunzi,Wanafunzi wenzao na mtu yeyote aliye ndani au/na nje ya shule.
9. Mwanafunzi anatakiwa aitike mwito wa kengele na mwito mwingine utakaoashiria kumhitaji kwa haraka na kwa nidhamu.
10. Mwanafunzi anaonywa kutumia lugha chafu kama Matusi, Kejeli, Vijembe, Mipasho n.k .
11. Mwanafunzi analazimika kuziheshimu na kuzitii alama za Taifa kama vile;-Bendera ya Taifa, Nembo ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Fedha ya Nchi, Sikukuu za Taifa n.k

12. Ni kosa kwa mwanafunzi kugomea adhabu halali inayotolewa na mtu mwenye mamlaka juu yake.
13. Mwanafunzi haruhusiwi kufuga kucha, kupaka rangi wala hinna.
14. Manukato ya aina yoyote (Perfumes) hayaruhusiwi kwa Mwanafunzi kwani huwasababishia wanafunzi wengine Magonjwa ya Mapafu kama vile Pumu.
15. Mwanafunzi anatakiwa kuonekana Nadhifu na katika Muonekano wa kawaida. Hivyo mapambo ya aina yoyote kama vile Hereni, Bangili, Mikufu, Culture (Kalcha) na Hirizi hayaruhusiwi.
16. Ni marufuku mwanafunzi kwenda kwenye nyumba za watumishi wa shule kwa sababu yoyote ile kwa muda wowote.
17. Wageni wa Wanafunzi hawataruhusiwa kuonana na Mwanafunzi siku za Masomo na/au Muda wa masomo. Mgeni yeyote anayetaka kumpa mwanae mahitaji,atayafikisha kwenye ofisi ya mwalimu wa zamu.
18. Ni marufuku kwa Mzazi/Mlezi, Ndugu, Jamaa au Rafiki kuwasiliana na Mwanafunzi kwa kupitia mawasiliano mengine zaidi ya yale yaliyo katika utaratibu wa shule.
19. Mwanafunzi haruhusiwi kufanya Mkutano bila kibali toka kwa Utawala au Uongozi wa Shule.
20. Mwanafunzi haruhusuwi kushiriki/kuendeleza Imani za kishirikina shuleni (mfano Mapepo, Marohani)
21. Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na fedha yoyote bwenini kwa ajili ya matumizi binafsi, fedha zote zinahifadhiwa kwa mhasibu wa shule na mwanafunzi atakuwa anachukua fedha yake ya matumizi kwa utaratibu maalum.

**NB:**

***Hizo ni baadhi tu ya sheria zinazotawala maisha na utamaduni wa shule. Nyingine utazifahamu ukiwa shuleni kadri ya muda na kuzoea maisha ya hapa shuleni.***

## 1. AHADI YA MZAZI/MLEZI

Mimi…………………………………………….Mzazi/Mlezi wa ……………………………………….
Ninakiri kuwa nimezisoma Sheria za Shule nikiwa na Mwanangu, tumezijadili kwa pamoja na tumezielewa. Ninakubali kushirikiana na Uongozi wa Shule katika kila kipengele cha Malezi ya mwanangu, na nitakubaliana na adhabu yoyote itakayoamuliwa na Uongozi wa Shule pale mwanangu atakapokiuka mojawapo ya Sheria na Kanuni hizi. Nitalipa ada, Michango ya Shule, na kuheshimu maelekezo mengine yanayotolewa na Shule.

Sahihi ya Mzazi/Mlezi ………………………………………..Tarehe:……………………………………..

## 2. AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi ……………………………………niliyechaguliwa Kujiunga na Kidato cha ……… katika Sekondari ya Kiislamu Vuchama Ugweno, nimesoma kwa makini Sheria na taratibu za Shule nikiwa na Wazazi / Walezi wangu. Nimejadiliana nao na nimezielewa vema kabisa. Ninahidi kuzitii, kuziheshimu na kuzishika wakati wote bila kusukumwa na nitakuwa tayari kuchukuliwa hatua kali za kinidhamu na Uongozi wa Shule endapo nitakiuka mojawapo ya Sheria na Kanuni hizi.

Sahihi ya Mwanafunzi:………………………………………...Tarehe:………………………………..

## 3. AHADI NA MAONI YA MKUU WA SHULE

Ninawaahidi ushirikiano wa dhati Wazazi / Walezi katika Malezi ya Mtoto wenu. Pia ninamtakia kila la kheri Mwanafunzi wangu huyu katika safari yake ya kielimu na maisha kwa ujumla.

**Karibu Sana Vuchama Ugweno Islamic Sekondari.**

______________________________

**MKUU WA SHULE**

***Wabillah Tawfiq***